

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Simu: 026-2322129

Nukushi: 026 -2322126

Baruapepe: [km@michezo.go.tz](mailto:km@michezo.go.tz)

Tovuti: [www.michezo.go.tz](http://www.michezo.go.tz)



Mji wa Serikali- Mtumba,  
Mtaa wa Michezo,  
S. L. P 25,  
**40481 DODOMA.**

*Dodoma,*  
**20 Februari, 2024.**

## TAARIFA KWA UMMA

### PONGEZA KWA RAMADHAN BROTHERS

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, **Mhe. Dkt Damas Ndumbaro (Mb)**, anawapongeza nyota wa sarakasi kutoka Tanzania, Fadhili Ramadhani na Ibrahim Jobu "**Ramadhan Brothers**" kwa ushindi mkubwa waliouopata katika Shindano la Vipaji liliofanyika nchini Marekani la "**America's Got Talent: Fantasy League**" ambapo katika shindano hilo wameibuka mabingwa na kuzawadiwa Dola za Marekani 250,000 ambazo ni sawa na shilingi milioni 637.5 za Kitanzania.

Dkt. Ndumbaro amesema ushindi wa Ramadhan Brothers umeitangaza na kuiletea heshima Tanzania Kimataifa na kuwa chachu kwa vijana wengine kuendelea kujituma katika kazi za Sanaa ambazo zimekuwa fursa ya ajira na chanzo cha mapato.

Amesema Ramadhani Brothers wanakuwa Watanzania wa kwanza kushinda mashindano hayo nchini Marekani. "Nawapongeza sana vijana hawa kwa ushindi waliouopata, wameonesha viwango vya hali ya juu, maarifa na kujituma licha ya kwamba wamewahi kushiriki mashindano hayo kabla" Amesema Dkt. Ndumbaro.

Ameeleza kuwa Ramadhan Brothers waliingia kwenye mashindano ya AGT kwa mara ya kwanza katika msimu wa 18 mwaka 2023 na kumaliza katika nafasi ya tano hatua iliyooungeza ari zaidi kwa vijana hao kuendelea kujituma ili wafanye vizuri zaidi.

Amesitisiza kuwa Serikali inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan itaendelea kuunga mkono kazi za Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kuweka mazingira rafiki na wezeshi kwa Watanzania ili waendelee kunufaika kiuchumi na fursa zilizopo hapa nchini.

Imetolewa na; -

A handwritten signature in blue ink, which appears to read "Aron Msigwa".

Aron Msigwa

**MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**